Bw. Spika, mimi si mtaalam wa maswala ya afya lakini uzoefu wangu na ujuzi wa kufanya kazi na jamii unanifanya nijue maswala mengi kuhusiana na akina mama na pia kwa yale mapenzi ambao niko nao, imenifanya nijue maswala mengi kuhusiana na janga hili ya saratani ya uzazi.

Bw. Spika, nimesikia maswala mengi yameulizwa ambayo hata wengine wamekosa kujua swala hili. Swala mojawapo ni kama lile swala ambalo limeulizwa ni umri gani ambao unaweza kufanya mama akawa anaweza kupata saratani ya kizazi. Ni mama ama mwanamke yoyote ambaye amebaleghe na amewahi kupitia swala la ngono ndiye ambaye anaweza kushikwa na ugonjwa wa saratani.

Kwa utaalumu, ukianza swala la ngono mapema zaidi unajihatarisha kwamba unaweza pata ugonjwa huu wa saratani haraka. Wale watoto ambao wanaanza swala hili mapema basi wajue wanahatarisha maisha yao. Hii ndio sababu Gavana wa kaunti hii alitoa amri ya kukataza watoto wasiende katika 'disko matanga.' Nafikiri kuna umuhimu wa hoja hii ipite na viongozi hususan wa jinsia ya kike wakiambatana na mimi balozi wa maswala ya akina mama, tuende pamoja kuwapatia hamasa akina mama hususan walio mashambani kujua ugonjwa huu hupakikana kupitia pale mwiba ulipochomea, kwa sababu wahenga husema 'mwiba uchemeapo ndio utokeapo.'

Hii saratani ya uzazi inatakikana ipimwe kupitia ile njia ya uzazi ili kuangalia kama mama ni kweli anaanza ugonjwa huu. Kina mama wengi wanaona vigumu Bw. Spika kuenda mahali, hata kama ni mwanamke mwenzake, kwenda kumfungulia miguu ili kupimwa ajulikane kama ana ugonjwa au la.

Haya yanataka watu ambao watakua wanaweza kutimbua majipu kueleza kina mama kinagaubaga ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anapimwa. Katika upimaji Bw. Spika, kama mama amepimwa, siku hizi kama ni mzima hana virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukimwi anatakikana apimwe kila baada ya miaka mitano, na kama ana virusi vya ugonjwa wa ukimwi anatakikana kupimwa kila mwaka. Hivyo basi, kama tulienda kwa uchunguzi na mama amepimwa anapatiwa karatasi na kuambiwa wakati wa uchunguzi mwingine ukifika, hakikisha umeenda kupimwa ili ujue kwamba uko sawa. Lakini iwapo atapatikana na virusi vya ukimwi huwa wanaharakisha ndio kila mwaka awe akipimwa. Inakuaje akina mama wanakubali hasa wale ambao bado wako katika umri wa uzazi kwenda kupanua miguu na kuwekwa chuma ili kuzuia... wakisema ni upangaji uzazi, lakini wanakataa kwenda kupimwa virusi vya ukimwi...

*(Hon. Kiraga stood on a Point of Order)*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. Kiraga:** Thank you very much. I am rising on a point of order under Standing Order No. 87 that the Mover gives us substantial evidence on two issues. One, the definition of cervical cancer; second, at what duration is one required to go for HIV test because I believe from the knowledge I have one is supposed to go for testing after a duration of three to four months.

Also on the definition of cervical cancer, this is where by the time a girl starts menstruation period that's the time when she can have this type of cancer. So unless he gives us substantial evidence on whatever he is trying to tell this House, I beg him to withdraw. Thank you.

**The Speaker (Hon. Kahindi):** Yes hon. Mwambire.

**Hon. Mwambire:** Bw. Spika, ingawaje ningependa kujibu maswali ambayo yameelekezwa na muhudumu maana yeye sio daktari, kama nimesikia lugha aliyoitumia vizuri amesema yule ambaye ameleta Mswaada huu ndio ajibu sio mimi niliyekuwa nikiongea. Kama ukinihusu nitanukuu maneno aliyosema mtoa hoja na mimi ninachangia Hoja ambayo imeletwa katika Bunge hili. Kwa hivyo sina wajibu wa kujibu swali hilo japo niko na majibu nayo. Nikienda kumalizia naomba wenzangu tuunge mkono swala hili na tuchukue wajibu wa kuhamasisha jamii kwa wingi kwa sababu kuna mashirika mengine yamejitokeza ya kuhamasisha kina mama.

Pia tujaribu kuangalia kile kitengo cha afya ndani ya kaunti hii kabla ya kutoa madawa, kuwe na mazungumzo ya kuhusu maswala ya afya, yapewa kipau mbele kila mahali waweze kuelezwa lakini kusiwe na urahisi...kwa sababu wamekuwa wakielezea kina mama mpaka ukifika katika zahanati, utaona ubao umeandikwa ni kina mama wangapi walijifungua hospitalini mwezi uliopita na ni kina mama wangapi wamefunga uzazi. Wale wanaofunga wazazi pia kuna vitengo vimeandikwa kuwa kina mama hawa wametiwa vidude vya mvingo ambavyo pia vinashindikwa kule ndani kwenye uzazi. Ni kwa nini kina mama wanakubali kirahisi kuwekwa kitu kama kile lakini wanakataa kupimwa saratani? Hilo ndio swali nililokuwa nikiuliza kabla sijasimamishwa. Tujaribu kukubaliana kwamba wale wahudumu wote wa afya ndani ya kaunti hii wahamasisha akina mama kuhusu swala hili nasi pia tulipatie heshima tukipata fursa yoyote ile; ni mazishini, harusini au mikutanoni kwa sababu ukweli hauna pazia.

Kwa hayo machache, nasimama kuunga mkono kwa dhati swala hili na ningepomba wenzangu msithubutu kupinga kwa sababu ukipinga ni kama kutoa mapenzi ya akina mama. Asante.

**Hon. (Ms.) Sophie:** Asante Bw. Spika. Kwanza wacha nimshukuru Mheshimiwa Mbeyu kutoka Kibarani kwa kuleta Hoja hii Bungeni. Saratani ya kizazi ni mbaya sana. Nasema hivyo kwa sababu nimeona kina mama wakiugua huku gharama ya matibabu ikiwa ya juu sana. Tukiwa nao tuwe mabalozi. Mimi nishaenda kupimwa na najua jinsi ambavyo unaweza kupimwa na ukimaliza ukajisikia uko sawa, kwa hivyo sio aibu. Ikiwa mtu anasema sisi huwa tunasikia aibu, mimi nasema sio aibu na ni vizuri ukija kuniuliza nitakueleza jinsi daktari atakuchukulia na mazungumzo mazuri na ujijue hali yako.

Ningetaka Bunge hili hasa akina baba muwahimize wake zenu maana iwapo saratani imempata itakuwa ni gharama juu yako. Tunafaa kuhamasisha watu wetu waelewe. Haina haja kutisha watu kuwa utapanuliwa. Kila mtu aelezwe kwamba huu ni ugonjwa na unaweza ukatibika. Asante sana.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. (Ms.) Tecla:** Asante, nami nimesimama kuunga mkono Mswaada huu. Ninampongeza sana mama Gertrude Mbeyu mheshimiwa wa wadi ya Kibarani kwa kuleta Mswaada huu Bungeni. Ni jambo la kupendeza alivyojua kwamba kina mama sana huwa wanashikika na matatizo mengi na zaidi saratani ikiingia kwa kizazi. Mara nyingi, ni sehemu nyeti, kwa matiti na hata sehemu za ndani mahali ambapo ikishika huwezi jua kwa urahisi. Maana kwa kawaida kama mama ama mwanamke ambaye tayari amebaleghe huwa anaenda kwa siku zake za kawaida na asijue ni nini kumbe huwa ni saratani inaanza. Kitambo kujua ni saratani, tayari huwa imemkula sana. Huwa kuna njia ambayo inatakikana ifanyike na kama alivyoongea tungetaka idara ya Afya iweze kutilia maanani jambo hili ili tuweze kuhamasisha akina mama kupitia kwa ushirika na wananchi ili wazuie magonjwa haya.

Kwa kufanya hivyo, kina mama watajijua mapema kuanzia umri mdogo hadi akina mama wazee. Kina mama wazee wengine wanafikia ule muda wao kuwa hawazai tena wala kupata zile hali za kike tena ashakuwa mtu mzima. Baadaye yanakuja kuchipuka mambo hayo kwa sababu haelewi chochote. Mama yule anaona ni kama anarudiwa na mambo ya kawaida. Ukimuuliza anakueleza mambo ambayo ni shida kwake na saratani itakuwa imeingia na oponyaji pale ni shida. Kwa hivyo, ningomba Bunge hili tuweze kuwa kitu kimoja tuweze kupitisha Mswaada huu ili kina mama wetu na sisi sote tuweze kupata hizi tiba na tukajielewe mapema ili wale kule chini mashinani waweze kupata hiyo elimu. Nawashukuru pia wale ambao walikuwa wanapinga Mswaada huu wamepata kuona kwamba kuna mwelekeo kuwa tunalenga akina mama ijapo kuwa hata wanaume pia wanazo saratani wanazozipata katika sehemu mbali mbali.

Hata hivyo, sasa tunalenga akina mama ambao sana sana huwa wanaumia kwa sababu ugojwa huu ukiwa uko ndani huwezi kuujua mapema. Kwa hivyo, nawashukuru wale wote ambao walikuwa wanapinga kwamba tusiendeleza Mswaada huu lakini pia nasema asante kwa Bunge lote kwa kuitikia mwito wa pamoja ili tuupitishie Mswaada huu. Asanteni.

**The Speaker (Hon. Kahindi):** Thank you. Yes, hon. Mramba.

**Hon. Mramba:** Asante sana Bw Spika. Nasimama kwanza kumpongeza Mheshimiwa Gertrude Mbeyu Mwanyanje ambaye ana nia ya kugombea kiti cha kuwakilisha akina mama kule Bungeni.

Pili, nawapongeza pia watu wa Kibarani kwa kutuletea mtu ambaye ana maono ya mbali. Mheshimiwa Spika, ninasimama kuunga mkono Hoja hii kwa sababu huu ugonjwa kwa kweli umeua kina mama wengi sana na wanaume pia wamekufa. Maanake nikizungumza pia mimi si daktari lakini wale madaktari wanaamini kwamba unapolala na mwanamke ambaye ana *cervical cancer* wewe pia unapata *prostate cancer*. Ndivyo ninavyojua mimi...

(Laughter)

... na haya ni maneno ambayo nimeelezwa na madaktari.

(Laughter)

Kwa hivyo, ikiwa hatutawaelimisha akina mama wakaenda kupimwa na kupata matibabu mapema sisi pia tumo hatarini kwa sababu huu ugojwa ni ugojwa ambao hasa wakigiriama huogopa...

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(Hon. Kiraga stood on a Point of Order)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes, hon...

**Hon. Kiraga:** Thank you very much Mr. Speaker. I have a very grave concern with the contribution of the hon. Member for Kakuyuni; that if you sleep with or you have sex with a lady who is suffering from that type of cancer you also automatically get that.

Mr. Speaker, I think we should get some clarification from the Member because from what I believe, cervical cancer is not a sexually transmitted disease unless he clarifies whatever he is trying to tell this House. So I beg him to withdraw because this is an honourable House. Thank you very much.

**Hon. Mramba:** Mheshimiwa Spika, siko tayari kuondoa maneno niliyoongea kwa sababu nimejulishwa na madaktari waliokwenda kusomea udaktari. Mheshimiwa Kiraga kwa bahati mbaya yeye ni mfanyikazi kwenye maabara ambayo ni *laboratory technologist*...

*(Laughter)*

Lakini hana ufahamu zaidi kupita hapo. Mheshimiwa Spika, madaktari wanaamini kabisa kuwa...

*(Hon. Foleni stood on a Point of Order)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Order! hon. Mramba. Yes, hon. Foleni.

**Hon. Foleni:** Asante sana mheshimiwa Spika. Nataka kumwelezea mheshimiwa ambaye amesimama kwamba swala ambalo limeelezewa na mheshimiwa Kiraga ni swala nyeti na linahitaji ufasaha na kujibiwa. mheshimiwa Spika, itakuwa ni utovu wa nidhamu kama mheshimiwa Mramba atasimama mbele ya Bunge hili ambalo ni Bunge tukufu na takatifu na aseme kwamba kile ambacho amesema mheshimiwa Kiraga hakistahili kupata majibu. Mheshimiwa Spika, kwa heshima mimi nami naomba mheshimiwa Mramba apeane jibu kwa lile swala mheshimiwa Kiraga alilosema.

Tatu, nimemnukuu msemaji mjumbe wa Kakuyuni kwamba mheshimiwa Mbeyu anatafuta kiti cha kuongoza akina mama. Ningeomba kujulisha Bunge hili kwamba sisi sote tunafahamu na hatuhitaji kuelezewa kwamba mheshimiwa Gertrude Mbeyu atawania kiti cha akina mama. Maneno haya yamesemwa na mheshimiwa Teddy Mwambire na yakarudiwa na mheshimiwa Nixon Mramba. Nasema hivyo kwa sababu tunaweza kubadilisha ziwe ni cheche za kisiasa kwa sababu si mheshimiwa Mbeyu peke yake ambaye anataka kuwania kiti cha akina mama. Kwa hivyo waheshimiwa wenzangu...

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Is that a point of Order or your submission?

**Hon. Foleni:** No! I was informing hon. Mramba that it is not in order...

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Okay hon. Foleni. As to the point of order which has been raised... take a seat hon. Mramba...It is a valid statement. What hon. Kiraga sought to know is; are these cancers sexually transmitted diseases? That is a question that doctors would be able to know. I am not a doctor myself and I have also not heard that they are sexually transmitted. Is it your position?

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(Clerk-at-the-Table consulted with the hon. Speaker)*

You know hon. Mramba, the statement you have made will be available to the entire public and in the next two weeks, somebody sitting in Germany or the USA will be watching what you are saying. I am concerned whether cancer is sexually transmitted. You have one option either to withdraw that statement or if you cannot substantiate now, we give you time you bring a document that will be... You know we are here as leaders because we intend to inform the public. We are not here to mislead the public. I have never heard of that; my mother passed on of cancer but my dad does not have cancer.

*(Laughter)*

I am also interested to know because I will also go back and advise my father and I think as leaders we need to be careful with what we say. Let me tell you something; Standing Order 87 makes you responsible for the statements that you make. It is good that you make the right choice of words. I am telling you that in the next two weeks, these proceedings will be streaming live to everywhere as long as somebody has internet on their phone or wherever it is.

If you have a colleague who lives outside the country then they will say; when did cancer become an STD, it is not HIV. So hon. Nixon Mramba it is business but it is not a joke. You either choose to substantiate or you withdraw because I am also interested to know if cancer is sexually transmitted.

**Hon. Mramba:** Mheshimiwa Spika, naomba niondoe matamshi hayo...

*(Laughter)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you very much. Now you can conclude on your submission. You have less than a minute to do so.

**Hon. Mramba:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono Hoja hii na tuzidi kutia mkazo zaidi kuelimisha akina mama zaidi na wale wasichana ambao wameanza kubeleghe ili waweze kujua kuwa kuna athari za ugojwa kama huu. Asante.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you very much.

**Hon. (Ms.) Nashee:** Asante mheshimiwa Spika. Naunga mkono ingawa naona sijui kutumia hii kompyuta maanake nimebonyeza kuanzia kitambo. Hata kina mama hawajaongea; hata mama zangu hapa waheshimiwa wawili pia hawajaongea. Nimeona wamewachwa nyuma; haidhuru mambo ni dijitali naelewa. Sasa, mimi naunga mkono Hoja hii na nampongeza mheshimiwa Mbeyu. Hata kama kuna mheshimiwa amesema tuwache kumpongeza mheshimiwa Mbeyu, lazima tumpongeze. Janga hili ni janga kubwa ulimwengu mzima. Ikiwa amelifikiria na yeye anataka kiti cha Mwakilishi wa kina mama Kilifi, lazima tumpe hongera tumjulisha kwa kweli uko na maono ya kuongoza watu. Hata kama wako ishirini na hata kama mimi nataka lakini nampa hongera kwa sababu amefikiria watu wake wa Kilifi kama mimi. Pia mimi nataka lakini sikuweza na hili ni janga kubwa ambalo limefikia ulimwengu mzima na limesumbua.

Waheshimiwa wenzangu, mimi nikiwa mmoja, nilienda kupimwa na kwa bahati mbaya nilisumbuliwa sana na hili janga na nikashikwa mpaka na presha. Nilipoenda kupimwa mara ya kwanza niliambiwa nimeshukiwa kama niko nayo na nikawa siwezi kulala; nikashikwa na presha

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mpaka nikaanza kufa upande mmoja. Kwa bahati nzuri, mara ya pili na ya tatu, nikaambiwa niko sawa.

Mimi naunga mkono vile mama yetu mheshimiwa Sophie amesema; wakati tutakapokuwa tukienda nyanjani ni vizuri kuwa wale waliopitia kwenda kupimwa wawe hapo waweze kuelezea mama zetu na wasichana wetu. Hata kama inaathiri wanaume, lakini akina mama ndio sana na tuweze kuwajulisha unapopimwa ukiambiwa huna ni bora na ukiambiwa uko nayo kuna dawa fulani kama haijakuwa imekaa sana kwenye mwili wako, unapewa hizo dawa kwa miaka miwili na inapotea kabisa. Na unapopewa kuna dalili zake unaelezewa kwamba ukiona dalili hii ujuwe unapona na ukiona dalili hii ujuwe inapona na ukiwa umeona dalili hii ujuwe hiyo bado iko, mpaka itafutiwe njia nyingine.

Kwa kipindi hiki kifupi waheshimiwa na mawaziri wameathirika na hili janga la saratani. Hata mimi pengine ningekuwa nimepotea hapa Bunge japo nataka nirudi. Sasa, mheshimiwa Spika, mimi namuunga mkono mheshimiwa Mbeyu na yeye kama anataka kiti cha Mwakilishi wa kina mama afikirie hivyo, alete Miswada kama hii nimfanyie kampeni. Nashukuru na ninaunga mkono.

**Hon. (Ms.) Arafa:** Thank you very Mr. Speaker, Sir. I stand to support this Motion and also congratulate hon. (Ms.) Mbeyu for coming up with this Motion, though it has taken a very long time since we went for recess. It has been very tricky, that is why hon. Teddy Mwambire and hon. Nzaro were trying to oppose the Motion. But it is not that it is a bad Motion but it has been more than two months since this Motion was tabled in this House.

Mr. Speaker, Sir, cervical cancer is one of the cancers that develop in women's cervix. It is an issue mainly touching on women and without the support of both men and women, it is very hard to overcome these challenges and there are different causes of cervical cancer; we have seen the issue of smoking and early sexually activities even to our young girls. It is not that all girls that are having sexual activities who have reached puberty, but even cases of rape can cause cervical cancer. We should not think that cervical cancer only targets old women, but different ages. Provided that you are a woman, you are at risk of having cancer.

There are different symptoms which we normally see or we think it is another disease like abnormal pain, vaginal bleeding and others. Sometimes women in the African culture feel very ashamed and sometimes I have experienced cases where men divorce their wives because they are undergoing these challenges, so it is not a role only for women but also men. I am very sure there are men here who are experiencing the same problem with their wives but they cannot ask their wives to undergo screening. It is not a role of women only but you can take your wives, you can take your daughter or any women who you think is undergoing the problem.

The National and County Governments are trying hard on the issue of HIV which is very bad. We have to go to these areas and even as leaders we need to lead by example. Every woman and man with their wives all undergo screening on cervical cancer and I am very sure Mr. Speaker, Sir, after some time, many people in Kilifi will adopt this. Charges for chemotherapy and surgery in cancer are very high, that is why our people are dying. Most of the times they are at a critical stage, to a point where they can not even take a month to survive. I am expecting every woman in this House to contribute to this Motion highly. We have been passing a lot of Motions in this House but implementation has been a big challenge and we want this Motion in favour of women in this County to be the first to be implemented. Thank you very much Mr. Speaker, Sir.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. Nzaro:** Thank you Mr. Speaker. First and foremost while supporting this Motion I want to dispel the fears that I was opposing it. What I wanted is to get more time so that we can incorporate the other cancers which have been mentioned by Members, because, personally my father died of prostate cancer. So in a way, I thought when we can incorporate the other types of cancers we will be making this Motion serve the people of this county better.

As you had indicated Mr. Speaker and I support this Motion because the prayer and what the hon. Member wishes to give the great people of this county is a way of preventing cancer. Personally as I have said we have these experiences. Treating cancer is very expensive. Today, I have a mother-in-law who is suffering from cervical cancer. I have been forced to in fact to send her for medication to a nearby country, in Tanzania because it is where those services are cheaper.

Mr. Speaker, these types of cancers are very preventable and it is only that you learn that you have cancer at a later stage but if you could have known earlier, then you could have sought preventive measures and maybe the cost of treatment would be cheaper. For the county as another Member said we should go for preventive measures rather than curative measures so this type of arrangement and the type of Motion which is before us seeks to address these issues. That is why I congratulate the Member for bringing this Motion to the Floor of the House.

In fact Mr. Speaker, there are some fears which have been allied that she is bringing this Motion because of political reasons. I think we should put sense in what we are trying to bring in this Assembly and the hon. Member is free to vie for any seat when the elections are called. It is also in order to congratulate her when she brings a Motion of this caliber and it tells us that she is fit even for a greater position in this country. Mr. Speaker, I support this Motion fully. Thank you.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you hon. Nzaro for your contributions.

*(Question, that the Mover now be called upon to reply, put and agreed to)*

**Hon. (Ms.) Mbeyu:** Thank you for giving me this chance to give my submissions. I want to take this opportunity to congratulate and thank every Member who contributed to this Motion. It was an excitement from my fellow MCAs from my mother Constituency Ganze. I am grateful that they read through the whole Motion and in between the line and realized the importance of this Motion.

I will not add much because much has already been said. I choose cervical cancer because it is a type of cancer that develops in women without notice and it is noticeable when it is already at a risky stage. I want to thank everybody. It is my prayer in Kilifi County that the Department of Health should have a programme to conduct an educational and informational campaign on cancer prevention, control and treatment. It is very important; my prayer does not mention campaign on women only it is campaign where women, girls and men get this information for better prevention, control and support for the women suffering from cervical cancer. Thank you Mr. Speaker for this opportunity.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you hon. (Ms.) Mbeyu for your submission. Hon. Members, a Motion has been tabled for debate and it has been deliberated. I now put the question.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(Question put and agreed to)*

**BILL**

*Second Reading*

**KILIFI COUNTY EMERGENCY FUND BILL, 2016**

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes hon. Mangi.

**Hon. Mangi:** Thank you Mr. Speaker. I beg to move that the Kilifi County Emergency Fund Bill, 2016 now be read a Second Time. I call upon hon. Daniel Chai Chiriba to second.

*(Hon. Chiriba stood at his place to second)*

Hon. Members, a Motion has been moved by hon. Mangi that the Kilifi County Emergency Fund Bill, 2016 be now read a Second Time. I do propose that the Motion is ready for debate

*(Question Proposed)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Chiriba.

**Hon. Chiriba:** Thank you for giving me this opportunity. I believe this hon. House knows the financial constraints that we are going through as a county. If we pass this Bill, it will give us access to funds and make the function run normally in the county. Mr. Speaker, I support and urge every Member to support the adoption as we look into the steps on how to implement the same.

**Hon. Gambo:** Asante mshemiwa Spika kwa kuniwezesha kusimama na kuunga mkono Mswada huu. Tumezunguka ndani ya kaunti hii kutafuta maoni na michango ya wananchi na wengi wameiunga mkono na kuweza kuchangia. Tunaposoma makadirio haya ya pesa yatawezesha kaunti kusonga mbele kwa kuwezesha mipangilio ya fedha ili ikaanze kufanya kazi. Naunga mkono Mswada huu uweze kusomwa kwa mara ya pili. Asante.

**Hon. (Ms.) Mbeyu:** Thank you Mr. Speaker. I rise to support the Second Reading of this Bill on the Emergency Fund. As you are aware, we have had tireless citizen participation on most Bills. Looking at the financial constraints, we want to believe this House has well dedicated and responsible Members who have been going round the whole county with just water during the public participation because we exhausted the funds. Issues are not working due to the monies which are stuck. I urge the Members to support the Bill. Thank you.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Members, a Motion has been moved by hon. Mangi to have the Bill read for the Second Time and the same has been deliberated. I now put the question.

*(Question put and agreed to)*

*(The Bill was read a Second Time and committed to the Committee of the Whole House at a later date)*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

...Thank you hon. Mangi.

*Second Reading*

THE KILIFI COUNTY PETITION TO COUNTY ASSEMBLY (PROCEDURE) BILL, 2016

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Mastaki.

**Hon. Mastaki:** Hon. Speaker, I beg to move that the Kilifi County Petitions to County Assembly (Procedure) Bill, 2016 be now read a Second Time. I call upon hon. Mwambire to second.

*(Hon. Mwambire stood at his place to Second)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you hon. Mastaki. Hon. Members, a Motion to have the Kilifi County Petitions to County Assembly Procedure Bill, 2016 has been moved in order to allow it to be read a Second Time. The same has been seconded by hon. Mwambire. I now propose that the same is ready for debate.

*(Question proposed)*

Yes, hon. Mwambire.

**Hon. Mwambire:** Thank you. I support the Second Reading of this Bill. This Bill gives us the validation of Chapter Six of the Constitution, whereby Members who serve in public offices should be vetted so that we get people of integrity.

Mr. Speaker, last time when we were vetting Members of the Executive and Chief Officers we had a difficult time because we did not have such laws in this county, that is why we used the national ones. We have a number of issues that need to be domesticated so that at least we can have people that we can have confidence in as a county, that they are people who are meeting the requirements as per the Constitution and the need of this county. That is why this Bill has come to address all issues pertaining to the validation of all exercises, so that in future when we will be employing people to office, we will be looking at specific areas before allowing somebody to get a position in this county. Thank you.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Members, a Motion has been moved to seek the Second Reading of this Bill. The same has been deliberated and now I put the question.

*(Question put and agreed to)*

*(The Bill was read a Second Time and committed to a Committee of the Whole House at a later date)*

Thank you hon. Matsaki for your contribution.

**ADJOURNMENT**

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Members, in the absence of any other business in the Order Paper today, I move to adjourn the House until tomorrow at 2:30 p.m. Thank you.

**The House rose at 4:16 p.m.**

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*